Miaka mitano ya kupunguza umaskini ilivyoleta neema vijijini

>>Mkurugenzi Mtendaji TASAF apongeza ushirikiano wa jamii kufanikisha miradi ya maendeleo



MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shadrack Mziray (Kulia), akimsikikiza Mzee Andrea Kwang' mkazi wa Kijiji cha Laja baada kupokea zawadi ya shuka ya kimasai na fimbo, wakati wa ziara ya viongozi wa TASAF walipotembelea Shule ya Sekondari Laja, iliyopo kijijini hapo, wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha. **(Na Mpigapicha Wetu)**

Na SULEIMAN JONGO

MARADHI ujinga na umaskini ni maadui wakuu wa Tanzania ambao vita dhidi yao ilitangazwa rasmi na muasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere, miaka ya mwanzo baada ya nchi kupata uhuru wake.

Kwa muda wote baada ya nchi kupata uhuru vita dhidi ya umaskini imekuwa endelevu, kila awamu kuanzia ya kwanza iliyoongozwa na Mwalimu Nyerere hadi ya sita tuliyonayo sasa, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeendeleza jitihada za kupambana na umaskini.

Kutekeleza kwa vitendo mkakati wa kupambana na umaskini, serikali chini ya Rais Dk. Samia imechukua hatua mbalimbali, mojawapo ni kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao umetekeleza Mradi wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Nne (Tanzania Poverty Reduction Program -TPRP IV).

Akitoa taarifa kuhusu utekelezaji na kufungwa kwa mradi wa TPRP IV, mbele ya waandishi wa habari Karatu mkoani Arusha, hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray alisema umekuwa na manufaa makubwa.

"Ninayo heshima kubwa kusimama mbele yenu leo kutoa taarifa ya mafanikio ya Mradi wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Nne (Tanzania Poverty Reduction Program -TPRP IV), ambao umekuwa mradi mahiri na wa kimkakati uliotekelezwa na TASAF.

"Mradi huu umechangia kwa kiwango kikubwa kuendeleza ajenda yetu ya maendeleo ya taifa, hususan katika kupunguza umaskini, kuboresha huduma za kijamii, na kuwezesha jamii nchini," alisema.

Alisema tangu kuanza kwa mradi huo Januari mwaka 2020, TPRP IV imejikita kimkakati kupunguza umaskini katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Njombe, Geita na Simiyu.

Lengo kuu lilikuwa kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na fursa za kuongeza kipato, hii imefanyika kwa kupitia ujenzi na ukarabati wa miundombinu iliyolengwa.

Mziray alisema mradi umewezesha ujenzi na ukarabati wa madarasa, vituo vya afya na vyanzo vya maji ambavyo sasa vinahudumia kaya za walengwa na jamii kwa ujumla.

Uwekezaji huo umeongeza upatikanaji wa huduma, umepunguza umbali wa kufikia huduma za afya na maji na kuimarisha mazingira wezeshi kwa ustawi wa jamii.

Pia, mradi huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha ustahimilivu wa kiuchumi. Kaya zilisaidiwa kutanua wigo wa vyanzo vya mapato kupitia shughuli kama ajira binafsi kwa sekta mbalimbali kikiwemo kilimo, ufugaji wa mifugo na shughuli nyingine za uzalishaji.

"Matokeo yake, familia nyingi zimeongeza kipato cha kaya, kuboresha usalama wa chakula na kuimarisha uwezo wa kukidhi mahitaji ya msingi," alieleza.

Alisema tathmini za karibuni zinaonesha kuwa TPRP IV imenufaisha kaya takriban 200,007 kwa kiwango cha mwitikio wa asilimia 96.7, jambo linalooneshа wigo mpana na athari chanya za afua za mradi.

Mojawapo ya mafanikio makubwa ni kukuza usawa wa kijinsia na kuunga mkono elimu ya wasichana. Ujenzi wa mabweni, vyoo na madarasa umeongeza uandikishaji, kuboresha udumishaji wa wanafunzi shuleni, na kupunguza mimba za utotoni.

Aidha, hatua hizo zimechangia kuboresha matokeo ya kielimu na kuongeza fursa kwa wasichana.

Alieleza kuwa, msisitizo wa ushirikishwaji wa jamii umejenga uwajibikaji wa pamoja na uendelevu, kuhakikisha rasilimali zinaendelea kufanya kazi na kutunzwa hata baada ya mradi kukamilika.

Pamoja na hayo, ushiriki wa wanawake umekuwa nguzo ya mafanikio, ambapo asilimia 56.5 ya kaya nufaika za mradi huo zinaongozwa na wanawake ambapo wanashiriki kikamilifu katika usimamizi wa miradi, akiba na uongozi.

MATOKEO CHANYA

Mkurugenzi Mtendaji Mziray, alisema jitihada za kuongeza kipato cha kaya zimeleta matokeo chanya, ikiwamo kaya nyingi kuongeza kipato kinachozidi sh. 200,000 wakati wa utekelezaji.

Vikundi vya akiba na shughuli za mikopo vimeziwezesha jamii, ambapo asilimia 88.3 ya kaya zina uelewa wa mifumo ya akiba na asilimia 38.9 zimepata ongezeko la upatikanaji wa mikopo, hivyo kuimarisha ustahimilivu wa kiuchumi na uhuru wa kifedha.

Mafunzo ya ujasiriamali yamefikia asilimia 82.4 ya kaya, yakichochea biashara mpya na kuongeza vyanzo vya kipato, hususan miongoni mwa wanawake wanaochukua nafasi za uongozi na kuanzisha shughuli endelevu za uzalishaji.

> ***Changamoto hizi zinatupatia masomo muhimu kwa siku zijazo. Tumejipanga kuzishughulikia kupitia ujenzi wa uwezo, kuimarisha ushirikiano, kuboresha mipango, na afua lengwa hususani kuendeleza uwezo na kurahisisha michakato ya usajili wa vikundi vya akiba kudumisha mafanikio na kupanua athari," alieleza.***

Mafanikio ya TPRP IV yamejengwa kupitia dhamira thabiti ya kisiasa katika ngazi za kitaifa na serikali za mitaa, ushiriki madhubuti wa jamii, na uratibu mzuri wa wadau.

"Tunaposherehekea mafanikio haya, pia tunatambua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, ukiwamo ucheleweshaji wa malipo na mahitaji ambayo hayakukidhiwa kikamilifu katika miundombinu ya maji na afya.

"Changamoto hizi zinatupatia masomo muhimu kwa siku zijazo. Tumejipanga kuzishughulikia kupitia ujenzi wa uwezo, kuimarisha ushirikiano, kuboresha mipango, na afua lengwa hususani kuendeleza uwezo na kurahisisha michakato ya usajili wa vikundi vya akiba kudumisha mafanikio na kupanua athari," alieleza.

Alisisitiza kipaumbele cha TASAFtu kinasalia katika uendelevu wa afua hizo, aidha wanapanga kuimarisha mifumo ya matengenezo, kupanua wigo hadi maeneo yenye upungufu wa huduma, na kuendelea kukuza ushiriki wa jamii.

Mziray alisema kuunganisha hatua za ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uwezo wa ndani kitakuwa kiini cha mkakati wa mfuko huo, kuhakikisha manufaa ya TPRP IV yanadumu na yanajumuisha wote.

Alifafanua kuwa, mradi huo umebainisha kuwa, maendeleo jumuishi yanayoendeshwa na jamii yanaweza kuleta manufaa ya kijamii na kiuchumi yanayoonekana, kupunguza vihatarishi, na kujenga jamii imara.

Mradi huo umeweka msingi imara wa maendeleo endelevu nchini kwa dhamira endelevu, upanuzi wa kimkakati, na ushiriki hai wa jamii, na kwamba kasi hiyo itaendelezwa kubadili maisha ya watu wengi, kukuza uwezeshaji wa kiuchumi, na kutimiza dira ya Tanzania yenye ustawi na usawa.

Kwa ujumla TPRP IV imekuwa na matokeo makubwa, yanayopimika ikiwamo kuchangia kusawazisha kipato cha kaya zenye uhitaji, kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu, na kuimarisha ustahimilivu wa tabianchi kupitia uundaji wa mali za jamii zinazochochea kilimo na uendelevu wa mazingira.

Aidha, mradi huo umewezesha uendelezaji wa ujuzi kwa wanajamii, kuwawezesha wananchi na kuimarisha uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo kwa ufanisi.

"Matokeo haya yanathibitishwa na takwimu za kina zinazoonesha manufaa halisi na mabadiliko chanya katika jamii zilizohudumiwa," alibainisha.

NINI KIMECHANGIA MAFANIKIO

Kanuni ya msingi ya TPRP IV ilikuwa kujumuisha jamii, wanajamii walishiriki kikamilifu kubaini vipaumbele, walichangia nguvu kazi, na walichukua umiliki wa mali zilizoundwa.

"Mchakato huu wa ushiriki umeongeza uhalisia na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa afua,"

Miongoni mwa mambo ya msingi ni kuzingatia ukamilifu kwa ulinzi wa mazingira na ushirikishwaji mpana wa wadau kuhakikisha miradi inakuwa salama, jumuishi na rafiki kwa mazingira huku uwajibikaji na uwazi ukiwekwa mbele.

Rasilimali kutoka Mfuko wa Jamii wa OPEC (OPEC Fund) zilitumika kwa shughuli zilizoidhinishwa, kwa mifumo imara ya ufuatiliaji, utoaji taarifa na ukaguzi, malipo kwa wanufaika yalifanyika moja kwa moja kama mishahara, yakihakikisha uwazi na heshima.

"Napenda kusisitiza majukumu yote ya kifedha na kiufundi yanayohusiana na TPRP IV yalitekelezwa kikamilifu, dhamira yetu ya kusimamia rasilimali za wafadhili kwa uwajibikaji inaendelea bila kuyumba," alisema.

Kwa mujibu wa Mziray, ujuzi uliopatikana unabaki kwa washiriki, na serikali za mitaa zimejipanga kuendelea kutunza na kuziunganisha mali hizo katika mipango ya maendeleo hatua ambayo itaiwezesha TASAF kutanua mbinu zilizofanikiwa, kuboresha mikakati kwa nia ya kuleta mafanikio Zaidi hususan katika awamu zijazo.

Mafanikio ya TPRP IV yamewezekana kupitia ushirikiano uliotokana na malengo ya pamoja kupunguza umaskini na kuunga mkono maisha endelevu.

"Tunatoa shukrani za dhati kwa OPEC Fund kwa msaada wao uliowezesha utekelezajhi wa mradi huu, ambao umekuwa nguzo muhimu ya kufanikisha matokeo haya. Ushirikiano wao ni mfano wa mbinu inayolenga matokeo na umechangia kwa kiasi kikubwa juhudi za maendeleo ya Tanzania," alisema.

MASHUHUDA WA MAFANIKIO

Moja ya miradi iliyotekelezwa kupitia mradi huo ni

Ujenzi wa shule bora ya kisasa katika Kijiji cha Laja, Halmashauri ya Wilaya Karatu, ambao umeibua shangwe na kuwapa tumaini jipya wazazi na wanafunzi wa kijiji hicho na vijiji vya jirani.

Wakizungumza mbele ya uongozi wa TASAF uliofika kijijini hapo kutembelea shule hiyo, walisema mradi huo umekuja wa

Christina Lucas mkazi wa kijiji hicho, alisema kabla ya kujengwa shule hiyo, wanafunzi hususan wasichana walikuwa wakiteseka kutembea kilometa nane kufuata shule kijiji kingine.

"Watoto wa kike ndilo kundi lililokuwa linaathirika mno kwa sababu wanakutana na adha nyingi kama ujauzito wa lazima na hivyo kukatiza masomo yao.

"Kwa hiyo ilikuwa changamoto kubwa iliyowaathiri watoto wengi kwani walikuwa wanaishia kidato cha pili kutokana na kupata ujauzito," alisema.

Akizungumza kuhusu TASAF, aliipongeza na kuishukuru kwa mradi huo na kusema umesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za jamii.

"Tunaendelea kutoa maombi kwa sababu muhitaji hachoki kuomba, ni kweli tunayo mabweni lakini bado tunahitaji maabara na nyumba za walimu kwani zilizopo hazitoshi. Tunatamani kama itawezekana basi Rais wetu Dk.Samia Suluhu Hassan kupitia TASAF atuone tena," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Laja, Daniel Panga, alipongeza juhudi zilizozaa shule hiyo hususan serikali chini ya Rais Samia kupitia TASAF na sasa faida yake inaonekana.

Alisema wanafunzi kukaa shuleni kumeleta tija kubwa ikiwamo kuwapa muda zaidi wa kujisomea.

Pia, wanafunzi kwa mazingira hayo hawawezi kuwa wazururaji wala kutoroka, "hivyo kwa kweli tunawashukuru wanakijiji wa Laja kwa kazi nzuri ambayo wametusaidia, bweni ni zuri wametusaidia. Maombi yetu ni kupatikana kwa maabara na kuongezewa nyumba za walimu."



MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shadrack Mziray (Kulia), akimsikikiza Mkuu wa Shule ya Sekondari Laja ya wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha, Daniel Panga wakati wa ziara ya viongozi wa TASAF shuleni hapo. **(Na Mpigapicha Wetu).**



VIONGOZI wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wakiwa katika Shule ya Sekondari Laja, Kijiji cha Laja wilayani Karatu Mkoa wa Arusha walipofika kuitembelea shule hiyo iliyojengwa kupitia Mradi wa Kupunguza Umaskini unaosimamiwa na mfuko huo**. (Na Mpigapicha**